Somo Kuhusu Rehema ya Mungu

YONA—SEHEMU YA 2

Maagizo: Fanya zoezi hili katika mazingira matulivu. Unaposoma maandiko, jiwazie ukiwa katika matukio yanayozungumziwa. Wazia kikao. Sikia sauti. Hisi kama wahusika wakuu wanavyohisi. Wazia kwamba masimulizi haya ni halisi kabisa.

❶ ***CHUNGUZA TUKIO HILI.—SOMA YONA 3:1–4:11.***

Unafikiria Yona alihisi jinsi gani alipokuwa akiingia katika jiji la Ninawi?_____

Unafikiria sauti ya Yona ilionyesha hisia gani alipokuwa akitangaza hukumu ya Yehova?_____

Inaonekana Yona alikuwa akisumbuliwa na nini alipokuwa ameketi nje ya jiji? (Soma Yona 4:5-8.)_____

❷ ***CHIMBA ZAIDI.***

Kwa nini huenda Yona alitaka Yehova aharibu Ninawi kama alivyokuwa ametabiri?_____

Ukitumia vifaa vya utafiti unavyoweza kupata, chunguza kuhusu **(1)** mmea wa mtango na jinsi ulivyoonekana, na **(2)** kwa nini mfalme wa Ninawi alijifunika nguo za magunia na kuketi katika majivu._____

Ingawa mwanzoni Yona alikataa kutoa unabii huko Ninawi, kwa nini anaweza kuitwa nabii mwaminifu na mwenye ujasiri? (Mathayo 21:28-31)

3 *TUMIA MAMBO ULIYOJIFUNZA. ANDIKA MAMBO ULIYOJIFUNZA KUHUSU . . .*

Uwezekano wa wanadamu kuacha maisha mapotovu.

Rehema ya Yehova.

Kwa nini tunahitaji kuonyesha rehema.

4 *NI MAMBO GANI KATIKA SIMULIZI HILI AMBAYO YAMEKUGUSA MOYO SANA, NA KWA NINI?*

Ili ufanye utafiti zaidi, ona gazeti la *Mnara wa Mlinzi* la Aprili 1, 2009 (1/4/2009), ukurasa wa 14-18.

www.jw.org © 2010 Watch Tower Bible and Tract Society of Pennsylvania